






## TAARIFA ZA HARAKA KUHUSU Essential Plan

### Je, nitajisajili vipi?

 [nystateofhealth.ny.gov](https://nystateofhealth.ny.gov)  
AU

 1-855-355-5777 au  
TTY: 1-800-662-1220  
AU

 Kupitia usaidizi wa ana kwa ana wa bila malipo kutoka kwa msaidizi aliyeidhinishwa karibu na nyumbani au kazini kwako.

### Je, mnaweza kunisaidia kwa lugha yangu binafsi?

Usaidizi unapatikana kwa lugha yako kwa simu na ana kwa ana.

### Ninaweza kujiandikisha lini?

Usajili kwa Essential Plan uko wazi mwaka mzima.

NY State of Health inazingatia sheria za haki za raia za Shirikisho zinazotumika na haibagui kwa msingi wa mbari, rangi, asili ya taifa, dini, jinsi, umri, hali ya ndoa/familia, rekodi za kukamatwa, hukumu za uhalifu, utambulisho wa jinsia, mwelekeo wa kingono, sifa za kinasaba, hali ya jeshi, hali ya mhanga wa unyanyasaji wa nyumbani, na/au kulipiza kisasi.

### Je, Essential Plan ni nini?

Bima ya afya kwa Wakazi wa jimbo la New York isiyo na malipo kwa wale wanaostahiki. Na inatoa manufaa sawa yaliyo msingi.

### Ni nani anayetimiza masharti ya kushiriki?

Watu wenye mapato ya chini ambao hawatimizi masharti ya kushiriki katika mpango wa bima ya Medicaid au Child Health Plus. Kuanzia Aprili 2024, sheria za kutimiza masharti ya kushiriki katika mpango wa Essential Plan zinapanuka na wakaazi zaidi wa New York watatimiza masharti ya kushiriki.

Ukubwa wa kaya	Pato la juu zaidi unaloweza kupata
1	\$37,650
2	\$51,100
3	\$64,550
4	\$78,000

### Je, inagharimu nini?

Malipo ya bima ya kila mwezi ni \$0 kwa wale wanaostahiki.

### Je, ni vipi vingine inavyo niokolea pesa ?

Haina DEDUCTIBLE (PUNGUZO), kwa hivyo mpango huu unaanza kulipia huduma yako ya afya mara moja.

Fidia za meno na macho zimejumuishwa bila uchangiaji wa gharama.

Unapata HUDUMA YA UZULIAJI BILA MALIPO kama vile chunguzi na kaguzi za daktari za mara kwa mara ili kukuweka mwenye afya.

### Je, Essential Plan inashugulikia nini?

Huduma sawia zinazotolewa na bima nyingine, ikijumuisha:

- kumwona daktari, ikijumuisha madaktari bingwa
- vipimo vilivyoagizwa na daktari wako
- dawa za kuandikiwa na daktari
- huduma za wagonjwa wa kulazwa na wa kurudi nyumbani katika hospitali
- na zaidi.

**HABARI NJEMA!**

**MPANGO WA ESSENTIAL PLAN UNAPANUKA ILI KUJUMUISHA WAKAAZI WENGI ZAIDI WA NEW YORK**

**KUANZIA APRIL 2024**